Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
Idara ya Habari - MAELEZO



# *Mwongozo kwa* Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari katika Kuripoti Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa *Mwaka 2025*

Julai, 2025

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 01 |
| Madhumuni ya Mwongozo | 02 |
| Wahusika wa Mwongozo | 03 |
| Kamati ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari Wakati wa Uchaguzi | 04 |
| Wajibu wa Idara ya Habari - MAELEZO | 06 |
| Wajibu wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) | 07 |
| Wajibu wa Vyombo vya Habari | 07 |
| Wajibu wa Waandishi wa Habari | 09 |
| Wajibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) | 11 |
| Wajibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi | 11 |
| Wajibu wa Vyama vya Siasa | 12 |
| Hitimisho | 13 |

# 1.0 *Utangulizi*

Katika muktadha wa uchaguzi ulio huru, wa haki na wenye kuzingatia misingi ya demokrasia, vyombo vya habari vina nafasi ya kipekee katika kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa umma. Vyombo vya habari ni daraja kati ya wagombea, vyama vya siasa, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na wananchi. Kwa kiasi kikubwa vyombo vya habari vinachangia katika kujenga uelewa wa wapiga kura kuhusu sera na ajenda za kisiasa, kuhamasisha ushiriki wa wananchi, na kuchochea uwajibikaji wa kisiasa ili kudumisha amani na demokrasia katika kipindi chote cha uchaguzi.

Hata hivyo vyombo vya habari vikitumika vibaya kuchapisha taarifa zisizo sahihi, au zenye upendeleo vinaweza kuvuruga amani na kuathiri haki ya wananchi kufanya maamuzi sahihi. Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024, kupitia kanuni zake, inatambua umuhimu na mchango wa vyombo vya habari katika uchaguzi.

Vilevile, Kanuni za Utangazaji wa Uchaguzi kwa Vyama vya Siasa ya Mwaka 2020 zilizoandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), zinaelekeza juu ya maadili, usawa wa maudhui, na udhibiti wa lugha ya uchochezi kwa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi.

Kwa kutambua wajibu huo mkubwa wa vyombo vya habari katika kipindi cha uchaguzi, Idara ya Habari - MAELEZO, kama taasisi inayoratibu utoaji wa taarifa rasmi kwa umma kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC), imeandaa mwongozo huu ili kutoa mwelekeo wa kitaaluma na wa kimaadili kwa vyombo vya habari katika kuripoti uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.

## 2.0 *Madhumuni ya Mwongozo*

Katika muktadha wa uchaguzi ulio huru na wa haki, mwongozo huu unalenga kuweka msingi wa kitaaluma na kimaadili kwa vyombo vya habari, waandishi wa habari na wahusika wote wa sekta ya habari katika kipindi cha uchaguzi, kwa madhumuni ya kuhakikisha haki, usawa, uwazi na weledi katika utoaji wa taarifa kwa umma ili kukuza demokrasia nchini. Kupitia mwongozo huu vyombo vya habari vitasaidia kulinda amani na utulivu wa taifa kwa kuepuka kuchapisha maudhui yenye viashiria vya uchochezi, upotoshaji au yasiyo na uthibitisho. Aidha, mwongozo huu unalenga kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi mabaya ya majukwaa ya habari ikiwemo mitandao ya kijamii, na kuhakikisha vyama vyote vya siasa na wagombea wanapewa fursa na uwakilishi sawia katika vyombo vya habari, kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia uchaguzi nchini.



# 3.0 *Wahusika wa Mwongozo*

**i. Idara ya Habari - MAELEZO**
Msimamizi mkuu wa Sekta ya Habari kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

**ii. Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB)**
Bodi hii ina jukumu la kuthibitisha sifa za kitaaluma za waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi watakaoshiriki kuripoti uchaguzi mkuu.

**iii. Vyombo vya Habari**
Vyombo hivi ndio vinavyoandaa na kusambaza maudhui mbalimbali kwa umma kwa lengo la kuelimisha au kuhabarisha hususan katika kipindi cha uchaguzi mkuu.

**iv. Waandishi wa Habari**
Waandishi wa habari wote waliothibitishwa na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari Tanzania wanaohusika na ukusanyaji, uchambuzi, utayarishaji, na usambazaji wa maudhui kwa umma, kupitia vyombo vya habari vya umma, binafsi, na majukwaa ya mitandaoni.

**v. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
TCRA imepewa mamlaka ya kisheria ya kusimamia sekta ya utangazaji nchini Tanzania.

**vi. Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC)**
Chombo chenye dhamana ya kisheria kasimamia uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani.

**vii. Vyama vya Siasa**
Vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992.

# 4.0 Kamati Ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari Wakati wa Uchaguzi

Katika kipindi cha uchaguzi mkuu, kutakuwa na kamati maalumu itakayofuatilia mwenendo wa vyombo vya habari katika kuzingatia weledi, maadili, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya uchaguzi. Kamati hii itasimamia uwajibikaji wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa kabla, wakati na baada ya uchaguzi kwa kuzingatia masharti ya mwongozo huu.

## 4.1 Muundo wa Kamati

Kamati ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari itaundwa na wajumbe wafutao:-

i. Mwenyekiti wa Kamati (kutoka Idara ya Habari - MAELEZO)

ii. Katibu wa kamati (atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe)

iii. Wajumbe wa kamati wakiwakilisha taasisi zifuatazo:-

a) Mwakilishi kutoka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

b) Mwakilishi kutoka Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari

c) Wawakilishi 2 kutoka vyombo vya habari vya umma

d)Wawakilishi 2 kutoka vyombo vya habari vya binafsi

e) Wataalamu 2 kutoka taasisi za elimu ya juu (vyuo vinavyofundisha uandishi wa habari)

f) Mwakilishi kutoka wizara ya mambo ya ndani na Jeshi la Polisi

g) Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

h) Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Mitandao ya Kijamii Tanzania (JUMIKITA).

i) Wawakilishi 3 kutoka vyama vya waandishi wa habari (TEF, UTPC, TAMWA).

## 4.2 Majukumu ya Kamati

Katika kutekeleza mwongozo huu Kamati ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari wakati wa uchaguzi itakuwa na majukumu yafuatayo:-

a) Kutathmini na kujadili mwenendo mzima wa vyombo vya habari katika kuripoti habari za uchaguzi;

b) Kufuatilia maudhui yanayotolewa na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi;

c) Kufuatilia uwiano wa taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi;

d) Kufuatilia utekelezaji wa sheria zinazohusu uchaguzi, na zinazosimamia sekta ya habari, kanuni na miongozo mbalimbali iliyowekwa;

e) Kuchukua hatua dhidi ya usambazaji wa habari potofu ambazo zinaweza kuleta taharuki, uchochezi ama kuharibu amani na utulivu wa nchi;

f) Kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusiana na utolewaji wa taarifa na habari za uchaguzi;

g) Kutoa mapendekezo ya hatua za kurekebisha dosari zitakazojitokeza wakati wa kuripoti uchaguzi;

h) Kutatua migogoro inayoweza kuibuka baina ya vyombo vya habari na wadau wengine wa uchaguzi;

i) Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mwongozo huu kwa vyombo vya habari na waandishi; na

j) Kuandaa ripoti ya kamati kuhusu utekelezaji wa mwongozo huu.

## 4.3 Uhai na Vikao vya Kamati

Kamati hii itaanza kazi mara INEC itakapotangaza rasmi ratiba nzima ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, na kumaliza majukumu yake baada ya kutoa ripoti yake mwezi mmoja baada ya uchaguzi kukamilika. Aidha, kamati hii itakutana mara moja kwa wiki katika kipindi cha uchaguzi mkuu. Endapo ikitokea dharula, kamati itakutana kwa ajili ya kushughulikia dharula iliyojitokeza.

# 5.0 *Wajibu ya Idara ya Habari - Maelezo*

Kama msimamizi wa vyombo vya habari vya uchapishaji, Idara ya Habari-MAELEZO ina wajibu ufuatao:

a) Kutoa na kusambaza kwa haraka na urahisi habari rasmi zinazohusiana na uchaguzi, ikiwemo ratiba, taarifa za vituo vya kupigia kura, takwimu za uandikishaji wapiga kura, na matangazo mengine kwa vyombo vyote vya habari vilivyoidhinishwa;

b) Kuratibu mawasiliano ya INEC na wahusika wengine wa uchaguzi kama waandishi wa habari, wizara, idara, na wakala husika wa serikali, ili kuhakikisha uwiano na uwazi katika mawasiliano rasmi;

c) Kupokea na kujibu maswali ya vyombo vya habari kwa njia zilizo wazi na zenye ufanisi;

d) Kusimamia uhuru wa habari kwa kuzingatia usalama wa taifa na utulivu wa nchi;

e) Kufuatilia maudhui yaliyomo kwenye magazeti na machapisho mengine ili kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni na miongozo mingine ya uchaguzi; na

f) Kupokea malalamiko yanayohusiana na maudhui ya vyombo vya habari vya uchapishaji katika kipindi cha uchaguzi na kuyawasilisha kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kusikilizwa na kutolewa maamuzi.

# 6.0 Wajibu wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB)

Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) ina wajibu muhimu katika kuhakikisha kwamba waandishi wa habari walioidhinishwa ndio pekee wanaoripoti uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani. Pamoja na mambo mengine, bodi itawajibika katika:

a) Kutoa vitambulisho maalum vya waandishi wa habari vilivyoidhinishwa, ambavyo ni lazima vioneshwe wazi wakati wa kutekeleza majukumu ya habari katika uchaguzi mkuu;

b) Kuandaa kanzi data ya waandishi wote wa habari wa ndani na je ya nchi walioidhinishwa kuripoti uchaguzi mkuu ndani ya mipaka ya Tanzania;

c) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa kanuni za maadili na mwongozo huu kwa waandishi wa habari na kushughulikia kwa haki na kwa haraka ukiukwaji wowote utakaojitokeza; na

d) Kusimamia mafunzo na kuwajengea uwezo waandishi wa habari kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu, vyombo vya habari na taasisi za mafunzo ili kukuza uelewa wa waandishi wa habari kuhusu kuripoti uchaguzi.

# 7.0 Wajibu wa Vyombo Vya Habari

Katika kutekeleza mwongozo huu, vyombo vya habari vitakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kuchapisha taarifa sahihi, zinazoweza kuthibitishwa, na zilizohakikiwa kikamilifu;

b) Kuepuka kubashiri, kueneza uvumi, kupendelea, na kuripoti madai yasiyothibitishwa ama yaliyotengenezwa makusudi kwa nia ovu kwa kutumia teknolojia ya kidigiti;

c) Kuepuka maudhui yenye lengo la kuleta chuki, ubaguzi, kashfa, matusi, kuchochea vurugu, au migawanyiko ya kikabila, kikanda, kidini, na kuhatarisha amani na usalama wa nchi;

d) Kuweka uwiano linganifu wa maudhui katika kuripoti habari au matangazo mbashara kwenye redio, runinga, na mitandao ya kidigiti hasa shughuli za kampeni, mikutano ya hadhara, na matamko kutoka kwa vyama vya siasa na wagombea wake;

e) Kuweka uwazi katika vipindi, matangazo au maudhui yanayolipiwa na vyama vya siasa. Tangazo lolote au maudhui yaliyolipiwa lazima yatambuliwe wazi na yasifichwe kama habari;

f) Kuhakikisha waandishi wao wa habari ambao wanahusika kuripoti uchaguzi wamepata ithibati rasmi kutoka bodi ya ithibati. Hii ni pamoja na waandishi wa muda, waajiriwa wa kudumu, na wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo wanaopangiwa kazi kipindi cha uchaguzi;

g) Kutoa taarifa kwenye Idara ya Habari – MAELEZO kuhusu aina yoyote ya vitisho, mashambulizi, usalama wa waandishi au vikwazo vya utekelezaji wa majukumu dhidi ya waandishi wa habari;

h) Kuhakikisha vinathibitisha uhalali na uaminifu wa taasisi zinazofanya tafiti za kura ya maoni kabla ya kuchapisha au kurusha taarifa hizo, ili kulinda usawa wa uchaguzi. Matokeo yoyote ya kura ya maoni hayapaswi kuchapishwa na vyombo vya habari (pamoja na mitandao ya kidigiti) ndani ya siku 30 kabla ya siku ya kupiga kura;

i) Vyombo vya habari vinavyopanga kuratibu au kurusha midahalo ya kisiasa vinapaswa kuhakikisha uendeshaji wake unazingatia sheria za uchaguzi na kutoa nafasi sawa kwa wagombea. Mipango ya midahalo hiyo lazima iwe wazi na jumuishi, na vyama vyote vya siasa pamoja na wagombea

wapewe taarifa na fursa ya kushiriki. Viongozi wa midahalo wasipendelee upande wowote, na wawe wabobezi katika kuendesha mijadala kwa weledi bila kuchochea migogoro;

j) Vyombo vya habari viepuke kurusha au kuchapisha matangazo ya kampeni, ujumbe wa kumuunga mkono mgombea, au maudhui yoyote ya kisiasa yenye mwelekeo wa kampeni kwenye magazeti, redio, televisheni na majukwaa ya kidigiti inapofikia ukomo wa kampeni kwa mujibu wa INEC;

k) Vyombo vya habari havitaruhusiwa kuwa na vituo vya kujumlishia matokeo, na badala yake vitapaswa kuripoti matokeo rasmi ya uchaguzi kutoka kwenye Tume Huru ya Taifa ya uchaguzi; na

l) Kuhakikisha kwamba, iwapo mwandishi wake wa habari atagombea nafasi yoyote na kushindwa kwenye mchakato wa uchaguzi, hatarudi kufanya kazi ya uandishi wa habari mpaka kipindi chote cha uchaguzi mkuu kitakapomalizika.

# 8.0 *Wajibu wa Waandishi wa Habari*

Katika kutekeleza mwongozo huu mwandishi wa habari atakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kuhakikisha kwamba amethibitishwa na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari ili kuripoti habari za uchaguzi;

b) Kuripoti habari na matukio yote ya uchaguzi kwa usahihi, bila upendeleo kwa chama, mgombea, au msimamo wowote wa kisiasa, na kuweka uwiano sawia wa taarifa kwa vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi;

c) Kutumia mbinu madhubuti za uhakiki wa taarifa (‘fact-checking’) kwenye majukwaa ya kidigiti na kwenye vyombo vingine vya habari;

d) Kuhakikisha kwamba habari zinazotolewa zimehakikiwa na kuhaririwa kikamilifu kabla ya kuchapishwa au kutangazwa;

e) Kuripoti kwa kuzingatia sheria za nchi, kanuni na miongozo yote inayosimamia sekta ya habari na utangazaji;

f) Kujiepusha kushiriki au kuunga mkono shughuli za kisiasa, kampeni, au mikutano ya vyama vya siasa ili kuepuka kuwa na upendeleo katika kazi yake ya kitaaluma;

g) Kutumia lugha ya Kiswahili au Kingereza katika kuripoti kampeni za uchaguzi isipokuwa itakapolazimu kutumia lugha nyingine kwa usaidizi wa mkalimani;

h) Kutoa uwakilishi sawa kwa makundi maaalum kama vile wanawake, wazee, watu wenye ulemavu, vijana, na wananchi wa vijijini kwa kuwapa nafasi kuelezea mitazamo yao bila upendeleo wowote;

i) Kuepuka upotoshaji wa taarifa binafsi au kusema uongo juu ya mgombea, chama, mtu, au taasisi yoyote inayohusika na masuala ya uchaguzi, au kutoa maoni yoyote yanayoweza kuleta chuki au uvunjifu wa amani;

j) Kuepuka kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji au vitisho katika kuripoti matukio ya uchaguzi;

k) Kuepuka rushwa, takrima au zawadi zenye lengo la kushawishi maudhui yenye kuegemea upande wa chama au mgombea fulani;

l) Kuchapisha au kutangaza habari zenye nia ya kuchochea vurugu, ubaguzi, au chuki za kisiasa, kikabila, kidini au kijinsi;

m) Kuepuka kufanya kampeni kwa namna yoyote ile katika siku ya kupiga kura, ikiwemo kuvaa mavazi yenye alama za chama au mgombea fulani;

n) Kuepuka kuingia katika vituo vya kupigia kura bila idhini maalumu, isipokuwa wale waliopewa kibali maalumu na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na

o) Kutochapisha matokeo ya uchaguzi kabla ya Tume ya uchaguzi kutangaza rasmi.

## 9.0 Wajibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Katika kutekeleza mwongozo huu TCRA itakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kuhakikisha vyombo vya habari vya kidigiti na vya utangazaji vinavyoripoti habari za uchaguzi mkuu vimesajiliwa au kuhuisha leseni zao kabla ya uchaguzi;

b) Kuhuisha au kusasisha Kanuni za Utangazaji wa Uchaguzi kwa Vyama vya Siasa 2020 ili ziendane na muktadha wa sasa na kuondoa mkanganyiko kwa watumiaji wa kanuni hizo; na

c) Kushirikiana na Kamati ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari wakati wa uchaguzi mkuu pamoja na taasisi nyingine zilizotajwa katika utekelezaji wa mwongozo huu.

## 10.0 Wajibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Katika kutekeleza mwongozo huu Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kutoa elimu kwa wapiga kura kupitia vyombo vya habari, ikijumuisha matangazo, midahalo na vipindi maalumu kwenye redio, mitandao ya kijamii na runinga Pamoja na makala kwenye magazeti

b) Kutoa taarifa kwa wakati kwa waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa uchaguzi ili kuepuka uvumi na habari ghushi;

c) Kuwezesha mafunzo mafupi kwa waandishi kuhusu sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uchaguzi ili kuimarisha uelewa wa taaluma yao; na

d) Kushirikiana na vyombo vya usalama kuhakikisha waandishi wanaripoti habari za uchaguzi katika mazingira salama.

## 11.0 *Wajibu wa Vyama vya Siasa*

Katika kutekeleza mwongozo huu chama cha siasa kitakuwa na wajibu ufuatao:-

a) Kumteua afisa au mwakilishi wake atakayekuwa anawasiliana na Kamati ya Ufuatiliaji wa Vyombo vya Habari wakati wa uchaguzi kuhusu utekelezaji wa mwongozo huu;

b) Kuwasilisha ratiba ya kampeni kwa wakati kwenye vyombo vya habari ikionesha eneo la uzinduzi wa kampeni, tarehe na muda;

c) Kuandaa na kuwasilisha makala au vipindi vyake vya kampeni kwenye vyombo vya habari na utangazaji kwa makubaliano na wahariri wakuu;

d) Kinaweza kulipia matangazo na vipindi baada ya kufanya makubaliano na vyombo vya habari;

e) Kuhakikisha kuwa kipindi ambacho kimerekodiwa kwa madhumuni ya kurushwa hewani hakina maudhui yanayoweza kusababisha chuki, uhasama na kuhatarisha amani;

f) Kuepuka kutoa machapisho yenye maudhui ya uzushi, uchochezi na lugha za kashfa;

g) Kuwaheshimu waandishi wa habari wanapokuwa katika mahojiano kwa kutoa majibu yenye staha; na

h) Kuwahakikishia usalama waandishi wa habari wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao.

# 12.0 *Hitimisho*

Mwongozo huu unasisitiza nafasi na wajibu wa vyombo vya habari, waandishi wa habari, wasimamizi wa sekta ya habari na wadau mbalimbali katika kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi na zenye uwiano sawia wakati wa kuripoti uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2025. Kwa kuzingatia misingi hii, vyombo vya habari vitachangia kwa kiasi kikubwa kulinda amani, utulivu, na demokrasia nchini. Wadau wote wanapaswa kuzingatia na kuheshimu miongozo iliyowekwa ili kuepuka upotoshaji, habari za uchochezi au ubaguzi ambazo zinaweza kuvuruga amani ya taifa. Ufanisi wa mwongozo huu unategemea ushirikiano wa karibu baina ya Idara ya Habari–MAELEZO, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari, vyombo vya habari, waandishi wa habari, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, vyama vya siasa na wananchi wote kwa ujumla.



Maelezo

Imesainiwa na;

Gerson Msigwa
Katibu Mkuu,
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
Julai 2025

Mwongozo kwa Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari katika Kuripoti Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025

Makole, Uhindini | S.L.P: 25 Dodoma
Namba ya Simu: +255 26 2322 129
Email: km@michezo.go.tz | www.maelezo.go.tz